# JARIDA

LA MTANDAONI | TOLEO LA JULAI - SEPTEMBA 2023

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

## Mkurugenzi Mkuu abainisha mafanikio lukuki, amesema yamechangiwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan




Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

Simu Bure 0800116773

@NssfTanzania



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba akifuatilia kwa ukaribu mwanachama aliyejiunga na huduma ya NSSF Taarifa Mobile App, ambapo mwanachama huyo aliweza kutazama michango yake bila kulazimika kufika katika Ofisi za NSSF

# NSSF ilivyotoa elimu ya hifadhi ya jamii kwenye Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam 'Sabasaba'.

**Na MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, alisema lengo la kushiriki maonesho hayo ni kutoa elimu ya hifadhi ya jamii, kuandikisha wanachama wapya kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kutangaza huduma mbalimbali zikiwemo za kidijitali kama vile huduma binafsi kwa mwanachama 'Member Portal', huduma binafsi kwa waajiri 'Employer Portal na WhatsApp Chat Bot. "Huduma zote hizi zinalenga kumrahisishia mwanachama wetu kupata taarifa zake popote alipo bila ya kulazimika kufika ofisini kwetu," alisema Mshomba.

Alisema kupitia maonesha hayo wanachama waliofika katika banda la NSSF waliweza kupata taarifa zao za michango, kufanya maboresho ya taarifa zao, kupata huduma zinazohusiana na masuala ya mafao yakiwemo ya muda mrefu ambayo ni Pensheni ya Uzee, Urithi na Ulemavu.  Pia, mafao ya muda mfupi ambayo ni mafao ya uzazi, kukosa ajira, matibabu na msaada wa mazishi.

Mshomba alisema NSSF pia ilitumia maonesho hayo kutangaza fursa za uwekezaji za Mfuko. "Kama mnavyofahamu hivi sasa Mfuko una miradi ya nyumba ambayo iko Dungu, Toangoma na Mtoni Kijichi jijini Dar es Salaam. Nyumba hizi zinauzwa kwa kila Mtanzania na bei yake ni nafuu. Vilevile tuna viwanja ambavyo vinauzwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa bei rahisi," alisema Mshomba.

# NSSF ilivyofikisha elimu ya hifadhi ya jamii katika Maonesho ya NaneNane

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulishiriki na kutoa huduma zake zote katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo 'Nane Nane 2023'. Maonesho hayo kitaifa yalifanyika katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya. Lakini NSSF pia ilishiriki maonesho hayo katika Mkoa wa Dodoma, Simiyu, Kagera, Tabora, Lindi, Mtwara, Morogoro, Mwanza na Arusha.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba alisema lengo la Mfuko kushiriki maonesho hayo ni kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kuandikisha wanachama wapya kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi kama vile wakulima, wafugaji, wavuvi, wachimbaji wadogo wa madini, mama lishe, bodaboda na wajasiriamali wengine wote, kutangaza huduma zetu mbalimbali zikiwemo za kidijitali kama vile huduma binafsi kwa mwanachama 'Member Portal', huduma binafsi kwa waajiri 'Employer Portal na WhatsApp Chat Bot.

Alisema pia wanachama waliotembelea banda la NSSF walipata taarifa zao mbalimbali zikiwemo za michango, kufanya maboresho ya taarifa zao na uhakiki kwa wastaafu wetu. Vilevile, Mfuko ulitoa huduma zinazohusiana na masuala ya mafao yakiwemo ya muda mrefu ambayo ni Pensheni ya Uzee, Urithi na Ulemavu. Pia tunayo mafao ya muda mfupi ambayo ni mafao ya uzazi, kukosa ajira, matibabu na msaada wa mazishi.



Meneja wa NSSF Mkoa wa Mbeya, Deus Jandwa (wa kwanza kulia), akiwahudumia wanachama wa NSSF waliotembelea banda la NSSF katika Maonesho YA Kimataifa ya Wakulima 'Nane Nane'




Mwanachama wa NSSF, Mussa Malubalo (kushoto) akipata elimu kuhusu mifumo ya kidijitali ya NSSF inayomuwezesha mwanachama kupata taarifa zake mbalimbali popote alipo bila kulazimika kufika katika Ofisi za NSSF



# NSSF ilivyoweka alama ya mafanikio Maonesho ya Madini

**Na MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, alimueleza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko kuwa NSSF ilishiriki Maonesho ya Sita ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini kwa sababu ndio Mfuko pekee wenye jukumu la kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi wakiwemo wachimbaji wadogo wa madini ili waweze kujiunga na kujiwekea akiba kwa ajili ya maisha yao ya sasa na baadaye.

Mshomba alisema tokea maonesho hayo yalipoanza mwaka 2018, NSSF imekuwa na mafanikio makubwa kwani ushiriki wake umechangia ukuaji wa Mfuko ambapo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2023, walikusanya michango ya takribani shilingi bilioni 56.

“Wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani, hapa Mkoani Geita pekee NSSF ilikuwa inakusanya michango ya shilingi bilioni 29 ambayo ni mara mbili katika kipindi hiki cha miaka miwili na nusu ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, kwa hiyo kwetu sisi ni mafanikio makubwa sana na tunaamini tutaendelea kufanya vizuri zaidi,” alieleza Mshomba.

# NSSF FUNGA KAZI

*** Mkurugenzi Mkuu abainisha mafanikio lukuki, amesema yamechangiwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan**

*** TEF yakoshwa na utendaji wa NSSF yapongeza kazi kubwa inayofanywa**

**Na MWANDISHI WETU**

Ni funga kazi pengine unaweza kusema hivyo! Baada ya Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba kubainisha mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa na Mfuko katika kipindi cha Machi 2021 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023.

Mshomba alisema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akitoa wasilisho la utekelezaji wa majukumu ya NSSF kati ya Machi 2021 hadi Juni 2023 kwenye kikao kazi baina ya Mfuko, wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari chini ya uratibu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR).

Alisema NSSF imefanikiwa kuandikisha wanachama wapya 547,882, kati ya tarehe 1 Machi 2021 na 30 Juni 2023 na kwamba idadi ya wanachama wachangiaji iliongezeka kwa asilimia 36 kutoka 874,082 tarehe 1 Machi 2021 hadi kufikia wanachama 1,189,222 tarehe 30 Juni 2023.

Kuhusu makusanyo ya michango alisema katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, kwa mwezi yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 97.67 iliyofikiwa tarehe 1 Machi 2021 hadi kufikia TZS bilioni 143.05 kwa mwezi katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023.

Hata hivyo, alisema makusanyo ya michango kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 43 hadi kufikia shilingi bilioni 1,718.28 katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ukilinganisha na shilingi bilioni 1,201.05 zilizokusanywa katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2021.

Alisema uwekezaji wa Mfuko pia uliongezeka kwa asilimia 111 kutoka shilingi bilioni 3,395.46 tarehe 1 Machi 2021 hadi kufikia shilingi bilioni 7,153.23 tarehe 30 Juni 2023.




Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba akizungumza katika kikao kazi kilichoratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kati ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Wahariri wa vyombo vya habari kuhusu mafanikio ya Mfuko yaliyopatikana katika kipindi kilichoanzia tarehe 1 Machi, 2021 hadi Juni 30, 2023




**Inaendelea ....**

Kati ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021 na mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023, thamani ya vitega uchumi vya Mfuko imekua kwa asilimia 55 hadi kufikia shilingi bilioni 7,153.23 tarehe 30 Juni 2023 kutoka shilingi bilioni zilizokuwa tarehe 30 Juni 2021.

Mshomba alisema katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, NSSF ilitumia wastani wa shilingi bilioni 61.93 kwa mwezi kulipa mafao mbalimbali kwa wanachama na wategemezi ikiwa ni ongezeko la asilimia 22 ukilinganisha na wastani wa shilingi bilioni 50.58 kwa kipindi kilichoishia tarehe 1 Machi 2021.

Aidha, kati ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021 na mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023 malipo ya mafao yaliyolipwa kwa wastaafu, wanachama na wanufaika wengine yaliongezeka kwa asilimia 25 na kufikia shilingi bilioni 743.17 katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023 ukilinganisha na bilioni 594.33 zilizolipwa Juni 30, 2021.

Naye, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deusdatus Balile amepongeza mafanikio mbalimbali ya NSSF yakiwemo ya ongezeko la michango, ongezeko la wanachama wachangiaji, ongezeko la mapato pamoja na ulipaji wa mafao.

# MATUKIO KATIKA PICHA - KIKAO KAZI CHA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA KATI YA NSSF NA WAHARIRI WA VYOMBO VYA HABARI
















Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF